# Mshukuruni bwana

## *Siku ya Mungu ya Kumi na mbili katika mwaka B*

Zaburi 106,21a.22a.24,25_26a.27b,28_29,30_3

Comp : Josué BANYWESIZE

Transc : Christoph Ntabaza






1, *Wamshukuru Bwana sababu ya wema wake,*
*na kueleza matendo yake kwa shangwe.*
*hao waliona matendo ya Bwana,*
*na maajabu yake vilindini.*

*2, Aliamuru, akavumisha upepo wa zoruba,*
*nao ukarusha juu mawimbi ya bahari,*
*wakapanda juu angani, wakashuka chini vilindini,*
*maarifa yao yote yakafutika.*

*3. Wakamlilia Bwana katika mahangaiko yao,*
*akawatoa katika masumbufu yao.*
*Akaituliza zoruba iwe upepo mwanana,*
*mawimbi ya bahari yaka nyamaza.*

*4. Wakafurahi kwakuwa yametulia,*
*akawapeleka katika bandari waliyotamani.*
*Wamshukuru Bwana kwa wema wake,*
*na maajabu yake kwa ajili ya wanadamu.*